# *Nahed Chapman New American Academy*

*1530 &* 1616 S. Grand
St. Louis, MO 63104
Office 314-776-3285
Fax 314-244-1711
Mwalimu Mkuu: Dr. Nicole Conaway
Saa: Mbili na dakika tano asubuhi hadi saa tisa na dakika na mbili
(8:05am - 3:02pm)
Gredi: K-8

**DAFTARI LA**

**MZAZI/MWANAFUNZI**



*Tunaamini Viongozi (LEADers) Hubadili Ulimwengu!*

*Nguvu yetu inatokana na unamnanamna!*

Wazazi wapendwa,

Ni furaha yangu kuwa Mwalimu mkuu wa Nahed Chapman New American Academy. Nikiwa mwalimu kwa zaidi ya miaka 20 na mama ya watoto wawili, ninaelewa umuhimu wa kuwa na mahali salama ili mtoto wako ajifunze na kukua.

Katika Nahed Chapman New American Academy, lengo letu ni kufanya jambo hilo hasa; tutaandaa mazingira salama, yenye upendo ambayo mtoto wako anaweza kujifunza stadi zinazohitajika za lugha ya Kiingereza ili afanikiwe Marekani na kwingineko.

Tumewajibika kufanya kazi pamoja na familia yako ili kuhakikisha kwamba mtoto wako ana hali bora zaidi shuleni. Ikiwa kuna jambo lolote tunaloweza kufanya ili kukutegemeza katika hatua hizi, tafadhali usisite kuwasiliana nasi.

Ninatazamia kufanya kazi pamoja na mtoto wako na familia yako.

Ni mimi,
Dr. Nicole L. Conaway

## Kwa nini Duma ndiyo nembo yetu?

Mwanzilishi wetu, Ms. Nahed Chapman, alikuwa mtetezi mkali ambaye aliwapigania kwa upendo watoto waliokuja kwetu kutoka sehemu mbalimbali za dunia. Ingawa alikuwa mpole katika mfikio wake, alitamani sana na alikuwa na bidii ya kutokeza njia ya kuwafundisha Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza katika Shule za Umma za St. Louis. Kwa hiyo, ingawa Duma ni wenye uwezo na wenye nguvu, hawangurumi au kuinua sauti zao.

## LENGO

Tunaamini VIONGOZI (LEADers) hubadili dunia!

## MAONO

Tutakuza sifa za uongozi (LEADership) kwa ajili ya mafanikio ya wakati ujao ya mtoto kwa ujumla.

## DUMA

Viongozi (LEADers) hubadili ulimwengu!
Mimi ni Kiongozi (LEADer)!
Mimi ni Mshikamanifu (Loyal).
Mimi ni mwenye Huruma (Empathetic).
Mimi ni mwenye Uthamini (Appreciative).
Mimi ninategemeka (Dependable).
Mimi ni Kiongozi (LEADer)!
Mimi ninabadili ulimwengu!

## 0FISI KUU YA NCNAA

**OFISI KUU YA NCNAA** inapatikana katika Jengo la 4 ambalo ni mlango ulio mkabala na Grand Avenue. Kwa ajili ya maswala yoyote yanayohusiana na shule, wazazi wanapaswa kuenda kwenye **OFISI KUU YA NCNAA**. Ikiwa wakalimani wanahitajika, wataitwa kwenye **OFISI KUU YA NCNAA**.

## TABIA INAYOTAKIWA

Wanafunzi wa Nahed Chapman New American Academy ni **Viongozi (LEADers)**!
Viwango vyetu vya uongozi ni **USHIKAMANIFU, HURUMA, UTHAMINI, na KUTEGEMEKA** (**LOYALTY, EMPATHY, APPRECIATION, and DEPENDABILITY)**.

Tunaamini kwamba ni muhimu kuwafunza wanafunzi jinsi ya kuonyesha Ushikamanifu, Huruma, Uthamini na Kutegemeka (Loyalty, Empathy, Appreciation and Dependability). Mambo Mbalimbali Yanayotakiwa yanaweza kupatikana mwishoni mwa daftari hii.

Shule za Umma za St. Louis zinaandaa ***Daftari ya Tabia Inayotarajiwa*** kwa kila mwanafunzi. Tafadhali pitia Daftari hii pamoja na mtoto(watoto) wako nyumbani. Ikiwa tabia ya mtoto wako itakuwa hangaiko, hatua za nidhamu zilizoorodheshwa katika Daftari ya Tabia Inayotarajiwa zitafuatwa.

## UHUDHURIAJI

Ili mtoto wako afanikiwe katika mwaka wa shule, ni lazima uhakikishe umetanguliza uhudhuriaji kwa ukawaida na kufika kwa wakati. Wanafunzi wakikosa kuhudhuria au wakichelewa kupita kiasi, inakuwa vigumu kwao kufuata maagizo ya kila siku wanapofika. Kuondoka mapema huathiri mafunzo. Wafanyakazi wa ofisini wanalazimika kuwakatiza na

kuwavuruga walimu wanapofundisha. Walimu wanalazimika kukatiza mafunzo ya siku na kutoa kazi ya kufanyiwa nyumbani na kuwasaidia wanafunzi wanaondoka mapema.

## KIAMSHA KINYWA

Kiamsha kinywa bila malipo huandaliwa kwa wanafunzi wote kuanzia saa moja na dakika arobaini asubuhi hadi saa mbili asubuhi (**7:40 am** until **8:00 am.**)
Wanapomaliza kiamsha kinywa, wanafunzi wataelekezwa kwenye chumba kimoja cha mazoezi shuleni, ambapo watasoma kitabu hadi kengele cha shule kitakapolia ili kuanza siku ya shule.  Mtoto wako anapaswa kubeba kitabu cha kusoma katika kipindi hiki.

## KUFIKA/KUONDOKA KILA SIKU

Darasa huanza saa mbili na dakika tano asubuhi kamili (8:05am)
Wanafunzi wataondoka saa tisa na dakika  mbili jioni (3:02pm)

Malango ya shule yatafungwa kila siku kwa ajili ya usalama wa wanafunzi na wafanyikazi.

Ikiwa ungependa kuingia, bonyeza kengele ya mlangoni. Unaporuhusiwa kuingia ndani ya jengo, tafadhali ripoti kwa Ofisi Kuu kabla ya kuingia darasani.

Wazazi hawataruhisiwa kuwaleta mtoto(watoto) wao **kabla ya saa moja na arobaini asubuhi (7:40 am)**. Wanafunzi wanapaswa kuachwa kwenye lango kuu karibu na jengo la kwanza (1).

Magari hayataruhusiwa kwenye chuo kuanzia saa moja na dakika arobaini na tano hadi saa mbili na dakika kumi na tano asubuhi (7:45 to 8:15 am) na baada ya shule kuanzia saa nane na dakika arobaini na tano alasiri hadi saa tisa na dakika kumi na tano jioni (2:45 until 3:15 pm) kwa sababu ya msongamano wa magari.

## KUONDOKA MAPEMA

Hakikisha kwamba unapoomba mtoto wako aruhusiwe kuondoka mapema, ni hali ya dharura. Kuondoka mapema hakuathiri masomo ya mtoto wako tu, bali huathiri wanafunzi wengine wote darasani.

Kuondoka mapema kutajumulishwa na kuhesabiwa dhidi ya rekodi ya uhudhuriaji ya mtoto wako. Kwa hiyo, isipokuwa mzazi(wazazi) wawe na taarifa ya daktari ya miadi, mtoto wako hataruhusiwa kuondoka shuleni kabla ya saa nane na dakika arobaini na tano (2:45 pm).

**HAKUNA mwanafunzi atakayeruhusiwa kuondoka na yeyote isipokuwa wazazi, walezi kisheria, au wale walioorodheshwa kuwa wanakubalika kuwachukua.**

**USIWATUME** ndugu, marafiki, au watu wengine wa ukoo walio chini ya umri wa miaka 21 kumchukua mtoto(watoto) wako. Watu wazima walioonyeshwa kwenye Fomu ya Kujisajili ndio tu watakaoruhusiwa kumchukua mtoto wako. Wanapaswa kuwa na picha ya utambulisho inayokubalika.

Utapigiwa simu ili kuthibitisha zaidi ombi hili, na ikiwa hutapatikana mtoto wako HATARUHUSIWA kuondoka.

Ikiwa utafika shuleni kumchukua mtoto wako kabla ya wakati wa kuondoka, lazima uripoti kwenye **OFISI KUU YA NCNAA** kabla ya kuingia darasani.

Katika jitihada za kuheshimu muda wa kujifunza, wanafunzi hawatatolewa nje ya darasa ili kupiga au kupokea simu. Jumbe zinaweza kupokewa.

## SIMU

Wanafunzi hawapaswi kuwa na simu ya mkononi shuleni. Ikiwa mwanafunzi ataonekana na simu ya mkononi ataonywa aindoe mara moja. Asipotii na simu hiyo ionekane tena, itachukuliwa na kuwekwa na Mwalimu Mkuu au Msaidizi wa Mwalimu Mkuu. ***Shule haitawajibika kwa kupotea au kuibiwa kwa simu za mkononi.***

## NGUO ZA SHULE ZINAZOFAA

Sare ya shule ni **LAZIMA** katika Nahed Chapman New American Academy.
Sare ya shule inatia ndani:

- Shati ya polo yenye kola ambayo ni rangi ya samawati hafifu, Nili, au Nyeupe yenye vifungo viwili
- Suruali ndefu ya rangi ya majani makavu au Nili
- Kaptula ya rangi ya majani makavu au Nili au sketi ya urefu unaofaa

Wanafunzi hawataruhusiwa **KUVAA** mavazi yafuatayo:

- Mavazi yanayoonyesha mwili kupita kiasi kama vile: sketi fupi, kaptula fupi, marinda mafupi/yanayobana, blauzi zenye mikanda inayofanana na tambi, blauzi zinazoonyesha mwili kupita kiasi
- Blauzi zinazoonyesha tumbo na/au kifua; suruali zenye mashimo; suruali zinazolegea kwenye kiuno na kuonyesha kaptula ya ndani, chupi au makalio
- Mavazi yanayotangaza pombe, tumbako, au vitu vilivyodhibitiwa, mavazi yenye lugha chafu, yanayorejezea ngono, ishara za magenge na kadhalika
- Mavazi mengine yoyote yanayobainiwa na Mwalimu Mkuu kwa kutegemea viwango vya shule

Maagizo ya ziada:

- Kofia za aina yoyote haziruhusiwi kuvaliwa ndani ya jengo la shule.
- Pindo za sketi zote hazipaswi kuwa juu ya kiwango cha ncha za vidole mikono inapowekwa kwenye pande za mwili.
- Blauzi au mashati lazima zichomekewe ndani ya suruali ndefu.

## KUTOKUWEPO

Ni muhimu kwamba mtoto wako ahudhurie shule kwa kawaida na kwa wakati kila siku ili ajifunze na kushika mambo makuu.
Ikiwa mtoto ni mgonjwa na hatakuwepo shuleni siku hiyo, tafadhali pigia Ofisi Kuu na uripoti kutokuwepo kwake. Wakati mtoto hayuko shuleni na hujajulisha **OFISI KUU YA NCNAA**, Mtaalamu wa Raslimali za Kijamii/Mzazi, Karani, Mshauri au Mfanyikazi wa Kijamii atawasiliana nawe.
Sheria ya jimbo inawataka wanafunzi WOTE wahudhurie asilimia 90% ya wakati wa shule. Wazazi watawajibika kifedha ikiwa kutokuwepo kunapita kiasi.

## HALI MBAYA YA ANGA

Stesheni ya radio ya **KMOX** na stesheni za televisheni zitaripoti kufungwa kwa shule kama ilivyoamuliwa na Mrakibu wa Shule.
Shule inapofungwa, **HAKUNA MFANYIKAZI aliye na zamu** katika Nahed Chapman New American Academy.

## SHERIA ZA BASI/MASHARTI

Wanafunzi wote watafuata sheria zilizowekwa na Sera ya Bodi ya Shule wanapoendesha mabasi kuelekea na kutoka shuleni. ***Wazazi na watoto wanapaswa kukumbuka, kutumia basi ni pendeleo, si haki yao, na jambo hilo linamaanisha pendeleo hilo linaweza kuondolewa ikiwa tabia ya mtoto inapelekea kuchukuliwa kwa hatua hiyo.***

USALAMA ndilo jambo la kwanza kuu wanafunzi wanaposafirishwa kuelekea na kutoka shuleni. Dereva anapaswa kukazia fikira barabara, na hapaswi kukengeushwa na mwenendo wa mwanafunzi yeyote.

Madereva wote watajaza Ripoti ya Nidhamu kuituma kwa Mwalimu Mkuu au Msaidizi wa Mwalimu Mkuu kuhusu mwanafunzi yeyote anayehatarisha usalama wa wengine kwenye basi anapoelekea shuleni/nyumbani.

Ikitegemea uvunjaji wa sheria, huenda wanafunzi wakakatazwa wasitumie basi kwa kipindi fulani cha wakati. Wanafunzi wanapokatazwa wasitumie basi, bado wanahitajiwa waende shuleni. Wazazi wana wajibu wa kumsafirisha mwanafunzi kuelekea na kutoka shuleni wakati wa kipindi cha Kukatazwa Kutumia Basi.

## VIFAA VILIVYOPOTEA AU KUIBIWA

Viwango vikubwa vya pesa, vifaa vya kuchezea, michezo, na/au simu za mkononi hazipaswi kuletwa shuleni.

Shule **haiwajibiki** kurudisha mali yoyote iliyoibiwa, pesa zilizopotea, au vyombo vyovyote vya kibinafsi vilivyowekwa vibaya/vilivyochukuliwa.

Shule **haiwajibiki** katika kuchunguza visa vyovyote vya vitu vilivyopotea au kuibiwa.

## DAWA ZA WANAFUNZI

Ikiwa inawezekana kwa vyovyote vile, dawa zinapaswa kupewanwa nyumbani.

Iwapo madawa lazima yatolewe shuleni na muuguzi wa shule, madawa **YOTE** yanapaswa kuwa na:

- ✓ Taarifa kutoka kwa daktari yenye ombi la dawa kutolewa shuleni
- ✓ Barua ya idhini kutoka kwa mzazi (inayotoka kwa muuguzi wa shule)
- ✓ Dawa **LAZIMA** ziwekwe katika chombo cha awali kilichokusudiwa dawa hiyo
  Jina la daktari na anwani ya duka la dawa

Dawa zinazotumwa shuleni bila taarifa ya daktari hazipaswi kutolewa shuleni.

Wazazi wanakaribishwa na wanatiwa moyo kuwapa wanafunzi dawa shuleni, wakati wowote inapowezekana.

## WATOTO WAGONJWA

Muuguzi wa shule, mwalimu mkuu, mshauri, au mfanyikazi wa kijamii atawasiliana nawe ili umchukue mtoto wako, umpeleke nyumbani na umsaidie apone, ili arudi shuleni akiwa mwenye afya nzuri.

Mzazi, mlezi au mtu anayepaswa kujulishwa kunapokuwa na hali ya dharura, ambaye ameorodheshwa katika Fomu ya Dharura ya Marejezo anapaswa kuja kumchukua mtoto mara tu anapojulishwa.

Mtoto wako **HATARUHUSIWA ACHUKULIWE** na yeyote ambaye hajaorodheshwa katika fomu ya dharura ya marejezo.

**Hakikisha kwamba una nambari ya simu inayotumika katika faili ofisini nyakati zote.**

## MIKUTANO YA WAZAZI

Mikutano ya wazazi inafanywa mara mbili katika mwaka wa shule, na ni muhimu sana uhudhurie.

Wazazi wanatiwa moyo waratibu na kutunza muda wa mkutano, ambao wamewekewa, pamoja na mwalimu wa mtoto wao.

Wazazi wote wanaagizwa waratibu mikutano ya mara kwa mara katika pindi zingine za mwaka, na vilevile kutembelea na kutazama katika madarasa ili waweze kuelewa zaidi jinsi Nahed Chapman Elementary inavyowasaidia watoto wao.

## WAJITOLEAJI

Wazazi, viongozi katika jamii, marafiki na watu wa ukoo wanaalikwa wajitolee katika Nahed Chapman New American Academy ambapo msaada wao unahitajiwa, na ni muhimu kwa ajili ya mafanikio ya watoto wote.

Tafadhali tembelea shule ili upokee ombi la mjitoleaji au wasiliana na Mtaalamu wa Kijamii na Familia kwa habari zaidi.

Mara tu unapoidhinishwa kuwa mjitoleaji, tafadhali rejezea Mtaalamu wa Kijamii na Mzazi, ukihakikisha kwamba unatia sahihi katika Faili ya Mjitoleaji inayopatikana katika ofisi kuu.

| *Tabia mbalimbali katika Shule Nzima ya NCNAA* | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Darasani** | **Ukumbi** | **Choo** | **Mkahawa** | **Basi** | **Kuwasili/Kuondoka** | **Uwanja wa michezo** |
| **Kiwango cha sauti** | Inategemea | 1 | 0 | 2 | 1 | 1 | Inategemea |
| **Ushikamanifu (Loyalty) (Wako, Wengine, Mali)** | Weka mikono, miguu na vitu kwako.<br>Uwe mwaminifu kwako na kwa wengine. | Tembea upande wa kulia. | Ingia/toka katika mpangilio mzuri.<br>Weka maji katika sinki pekee.<br>Tumia vizuri raslimali za bafu.<br>Safisha baada ya matumizi yako binafsi na ya wengine. | Chagua chakula haraka.<br>Baki katika foleni iliyonyooka.<br>Safisha baada ya matumizi yako binafsi na ya wengine. | Msikilize dereva kwa makini.<br>Keti ukitazazma mbele.<br>Weka mikono na vitu vingine ndani ya basi.<br>Baki ukiwa umeketi wakati wote wa safari.<br>Weka mikoba ya juu ya mapaja yako. | Ingia ndani ya basi na ushuke taratibu.<br>Angalia kabla ya kuvuka barabara.<br>Ingia ndani ya basi na uketi bila kukawia. | Tumia vifaa kwa njia inayofaa.<br>Fanya maamuzi salama. |
| **Huruma (Empathy)** | Sikiliza wengine wanapoongea na usubiri zamu yako. | Tabasamu na uwapungie wengine wanaokupita mkono. | Ikiwa kuna mtu anayehitaji msaada, mweleze mtu mzima. | Keti pamoja na marafiki mbalimbali.<br>Wakaribishe wengine walioketi peke yao wajiunge na wewe. | Watafute wanafunzi wanaohitaji msaada na uandae msaada. | Unaposhuka kutoka kwenye basi, subiri zamu yako.<br>Waruhusu watoto wadogo waingie na kushuka kwanza. | Jiruhusu na uwaruhusu wengine wafanye makosa.<br>Wahusishe wengine. |
| **Thamini (Appreciation)** | Tumia lugha chanya na inayofaa. | Tembea ukiwa kimya.<br>Usirushe rushe mikono.<br>Usishike ubao ulio kwenye maeneo ya kutembelea. | Usiwaangalie wengine.<br>Okota taka na uzitupe kwenye pipa la taka.<br>Vuta maji baada ya kutumia choo.<br>Tembea kwa makini.<br><br>Funga maji. | Fuata mwelekezo wa wafanyikazi mara ya kwanza tu baada ya kutolewa.<br>Tumia lugha chanya.<br>Sema tafadhali na asante. | Ingia kwenye basi kwa mpangilio mzuri.<br>Tumia lugha chanya na inayofaa.<br>Msikilize dereva wa basi kwa makini.<br><br>Okota taka na uzitupe kwenye pipa la taka. | Tumia lugha chanya na inayofaa.<br>Toa kofia zilizoshonewa kwa koti na kofia unapokuwa ndani ya jengo. | Shiriki.<br>Subiri zamu yako.<br>Uwe na maoni chanya hata unaposhindwa-Asiyekubali kushindwa si mshindani. |
| **Kutegemeka (Dependability)** | Fanya yote uwezayo.<br>Fuata miongozo mara ya kwanza inapotolewa. | Enda moja kwa moja katika darasa lako.<br>Nyakati zote upite.<br>Okota taka iliyo kwenye pipa la taka. | Ripoti visa vya maandishi ukutani au kujeruhiwa kwa wafanyikazi.<br>Tupa taulo za karatasi ndani ya pipa la taka. | Unapoagizwa, safisha eneo lako na utupe taka.<br>Kariri nambari yako ya mwanafunzi. | Panda basi lako.<br>Hakikisha ndugu na dada wako ndani ya basi. | Subiri kimya kupokea maagizo mkiwa katika mstari mmoja.<br>Fika dakika 10 mapema kwenye kituo cha basi.<br>Vaa sare yako ya shule.<br>Fika shuleni ukiwa umejiandaa na vifaa vyako vyote. | Tunza vifaa vyako. |